COVID-19 RESPONSE

UN environment programme




# Kushirikiana na Mazingira ili Kuwatunza Binadamu

## Jinsi UNEP inavyokabiliana na COVID-19

**Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) linasimama na mabilioni ya watu wanaoteseka kwa sababu ya janga la COVID-19. Tunatanguliza kuwalinda. Lakini UNEP pia inawajibu wa kusaidia mataifa kujijenga tena kwa njia bora baada ya janga ili kuongeza ustahimilivu kwa majanga ya wakati ujao.**

COVID-19 inaonyesha kwamba afya ya watu na sayari ni sawa. Shughuli za binadamu zimegeuza kila pembe ya Dunia, ikileta wanadamu karibu na wadudu wa kuuma wapya: asilimia sabini na tano ya magonjwa ya kuambukiza yanayotokea kwa wanadamu yanatoka kwa wanyama. Tishio ya muda mrefu ya mabadiliko ya hali ya hewa na ikolojia na kupoteza viumbe anuwai pia inatokana na uharibifu wa asili.



Wazo la dunia asili inayositawi ni muhimu kwa afya ya wanadamu, jamii na uchumi wakati wote imekuwa jambo kuu kwa kazi ya UNEP. Lakini sasa UNEP lazima iandae utegemezo zaidi kwa nchi wanapopunguza hatari ya majanga ya wakati ujao kwa kurejesha ikolojia na viumbe anuwai vilivyopotea, kupigana na mabadiliko ya hali ya hewa na kupunguza uchafuzi.

UNEP itategemeza mataifa na washirika kutoa sayansi yenye nguvu zaidi, sera inayotegemeza sayari yenye afya zaidi na uwekezaji wa kufaidi mazingira kupitia jukumu lake la msingi na Programu ya Kazi. Itapanuka na kutia nguvu ushirika na mashirika mengine ya UN ili kushughulikia mahitaji ya nchi wanapokuza Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mkataba wa Paris na mikataba mingine muhimu. UNEP itafuatilia mageuzi ya haki kuelekea mifano mipya ya kiuchumi inayolinda maskini na wanyonge wa dunia- kwa kuwa watu hawa ndio wanaoteseka zaidi kutokana na majanga na uharibifu wa mazingira.

Katika COVID-19, sayari imetoa onyo kali hadi sasa kwamba wanadamu lazima wabadilike. Kufunga uchumi ni itikio la muda mfupi kwa onyo hili. Haiwezi kudumu. Kwa kujenga uchumi unaofanya kazi na nguvu za asili, na sio dhidi yake, ndipo tu mataifa ya dunia yanaweza kusitawi.

**— Inger Andersen,**
Mkurugenzi Mkuu wa UNEP



**Inger Andersen**
Executive Director of the United Nations Environment Programme and Under-Secretary-General



***“In COVID-19, the planet has delivered its strongest warning to date that humanity must change”***

# MUKTADHA

Hati hii inapaswa kusomwa kwa muktadha wa ripoti ya Katibu Mkuu kuhusu Athari za COVID-19 kwa Jamii na Uchumi na mfumo wa Kikundi cha Maendeleo Endelevu cha UN cha itikio la moja kwa moja la jamii na uchumi kwa COVID-19. Kutegemeza mataifa yanayoshiriki katika jitihada zao kushughulikia athari za COVID-19 kwa jamii na uchumi na mazingira, UNEP itafanya kazi na mifumo yote ya UN kuandaa utegemezo unaohitajika kwa mataifa yanayoshiriki. Pointi mbili zifuatazo kutoka kwa ripoti ya SG zinahusiana hasa na majukumu ya UNEP:

- **Agenda ya 2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mkataba wa Paris kuhusu Kubadilika kwa Hali ya Hewa bado ndio fursa yetu bora kwa wakati ujao mwangavu.** Iwapo tungechukua hatua upesi ili kuchughulikia michakato hii, ulimwengu ungeweza kukabiliana na COVID-19 kwa njia rahisi–ulimwengu ungekuwa na mifumo ya afya iliyoimarishwa, watu wachache wanaoishi kwa ufukara, kiwango cha chini cha ubaguzi wa kijinsia, mazingira mazuri na jamii yenye ustahimilivu zaidi.
- **COVID-19 haiandai 'matumaini' kwa mazingira, lakini inaandaa motisha kuangalia tena uhusiano wetu na mazingira asili na kujenga dunia bora.** Serikali zinapaswa kukabiliana na janga la COVID-19 kwa kuunda sera na kufanya maamuzi ya uwekezaji ambayo pia inashughulikia majanga kama vile uchafuzi wa hewa na dharura ya hali ya hewa. ■



### ITIKIO LA KWANZA 1:

## Awamu ya dharura ya matibabu na fadhila


**Athari mbaya kwa afya ya wanadamu na kwa sayari itatoka kwa vyanzo vingi wakati dunia inakabiliana na COVID-19: ongezeko la taka hatari- kama vile vifaa vya kujikinga, vifaa vya elektroniki na dawa; mamilioni ya lita ya maji taka, na matumizi makubwa ya sabuni, vipukusi na miyeyusho yenye kuua vijidudu. UNEP itakabilian na changamoto hizi zinazotokea kupitia:**

- **Maarifa, habari na uhamasishaji** – Kuelimisha wanaofanya uamuzi muhimu jinsi ya kukabiliana na taka za kimatibabu kutokana na covid-19, kwa kuzingatia zaidi matumizi ya rasilimali kikamilifu na uzalishaji wa bidhaa zinazoweza kutumiwa tena na tena.
- **Tathmini ya uwezo wa usimamizi wa taka ya matibabu ya nchi –** Kuwasaidia wanaotengeneza sera kukuza mikakati ya muda mfupi kutumia kabisa uwezo uliopo na, kwa muda mrefu, kutegemeza tathmini ya kitaifa ya uwezo wa usimamizi wa taka ya kimatibabu kusaidia mataifa kushirikisha mikakati ya taka ya janga kwa utayari wa kipeo na itikio.
- **Sera na mifumo ya kisheria ya usimamizi wa taka iliyochafuliwa ya COVID-19** – Kutathmini sheria za kusimamia taka na kukuza mwelekezo unaofaa changamoto za COVID-19.

»

- **Kutenga, kuainisha, kuhifadhi na kuweka akiba taka ya COVID-19 –** Kukuza teknolojia na mbinu bora kwa mazingira za usimamizi wa taka – ikiwa ni pamoja na suluhisho la muda la kuweka akiba taka na kuzuia kutupa au kuchoma wazi, ambayo huenda ikasababisha matatizo zaidi ya afya.
- **Miundo msingi mpya na uwezo–** Kutegemeza mataifa kujenga miundo msingi mipya ya kukabiliana na taka za matibabu. Ukosefu wa upatikanaji wa teknolojia ya hali ya juu ya kutibu uchafu wa matibabu uliochanganywa huzua changamoto kubwa kwa nchi nyingi zinazoendelea. ■

*Ijapokuwa kuna hoja ya kushughulikia hali kiutu, ni sharti serikali zishughulikie mazingira*




ITIKIO LA KWANZA 2:

# Badiliko lenye mageuzi kwa asili na watu

Sayari yenye afya ni muhimu kwa uwezo wetu wa kurudi kutoka kwa janga la COVID-19 na kuzuia magonjwa yanayotoka kwa wanyama ambayo husambaa kutoka kwa wanyama hadi kwa binadamu. Kuzorota kwa mifumo ya ikolojia, na viumbe anuwai ndani yake – kupoteza makazi na muundo, ukuzi wa kilimo, mabadiliko ya hali ya hewa, uchafuzi, na kutumia spishi vibaya- inaongeza hatari ya majanga ya magonjwa kutoka kwa wanyama. Itikio la UNEP kwa changamoto hizi litaangazia:

- **Kuboresha kwa sayansi na sera ili kuelewa vyema na kukabiliana na magonjwa kutoka kwa wanyama** – Kuunda programu ya kukabiliana na magonjwa yanayotokana na wanyama inayolenga kuboresha uwezo wa nchi kukabiliana na magonjwa hayo bila kudhuru mazingira. Hii ni pamoja na sera za kisayansi; juhudi mpya za kimataifa za kupunguza madhara yanayotokana na kutokuwepo na sheria dhidi ya bidhaa zinazotokana na wanyamapori, unyakuzi wa maeneo ya makazi na uharibifu wa bayoanuai; na itikio lililopanuliwa ya sera inayoendana na mahitaji ya mataifa.

- **Kuwekeza katika asili ili kuboresha afya ya wanadamu, urejesho endelevu wa jamii na uchumi, kupunguza umaskini na urejesho wa mapato** – Kukuza fursa zaidi za kukadiria thamani na uwekezaji kwa asili kama sehemu ya itikio kwa janga la COVID-19.
- **Sayansi, msaada wa kiufundi na utetezi kuhakikisha maendeleo katika maswala ya mazingira kupitia michakato ya ulimwengu** – Kutegemeza mataifa kuandaa ahadi zenye nguvu chini ya Mkataba wa Paris, kukubaliana na Mfumo wa Viumbe anuwai ya Ulimwengu wa baada ya 2020, na kutwaa Mfumo wa Usimamiaji wa Kemikali na Taka baada ya 2020. Kuwasaidia kutoa ahadi zilizotolewa kwa michakato hii na mingine.
- **Kuhamasisha kuhusu uhusiano kati ya mazingira asili, afya na maisha endelevu–**Kuhamasisha umma kuhusu uhusiano kati ya mazingira na afya ya binadamu, kutengeneza utegemezo wa umma kwa ajili ya fursa za kukuza njia ya kupunguza athari mbaya kwa mazingira ndani ya urejesho wa uchumi, na kutetea maisha endelevu na chaguo bora kupitia kampeni za mawasiliano na jukwaa za elimu.
- **Masomo kuendelea** – Huku zaidi ya wanafunzi bilioni moja wanaposalia nyumbanina kushindwa kwenda shuleni, UNEP imekuwa ikishirikiana na viongozi katika elimu ya masuala ya mazingira kuanzisha “Earth School”, vipindi vya ubunifu vinavyoendelezwa na TED-Ed. UNEP pia itashirikiana na Mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, taasisi za elimu na serikali ili kujumuisha mada kuhusiana na mazingira kwenye mitaala ili kusaidia ulimwengu “kusoma vizuri tena”



***Zaidi ya vijidudu vipya 30 vinavyoambukiza binadamu magonjwa vimegunduliwa kwa kipindi cha miongo mitatu tu iliyopita. Jumla ya asilimia 75 hutoka kwa wanyama. Janga hili halipaswi kujirudia tena.***

## ITIKIO LA PILI 2: HAZINA MUHIMU NA MIRADI

- **Fedha ya Amana ya Wadau Wengi ya Muongo wa UN juu ya Urejesho wa Ikolojia –** Itachochea uchumi mpya wa marejesho kutoa ajira na kuongezeka kwa ugavi bidhaa na huduma kutoka kwa mfumo wa ikolojia wenye afya.
- **Kituo cha Msaada wa Mbegu ya Mtaji kwa ajili ya Urejeshaji wa Misitu na Mazingira cha Ulaya –** Kwa sasa EUR milioni 25, kituo kitaangazia juu ya utengenezaji wa ajira na ajira vijijini katika maeneo ya kipaumbele yaliyoathiriwa pakubwa na janga la sasa au walio chini ya tishio
- **Hazina ya Ustahimilivu ya Jamii –** Kwa kutumia EUR milioni 20, hazina hii itaandaa misaada midogo kwa jamii ili kujenga tena jamii zenye ustahimilivu kwa kutumia suluhisho la asili.
- **Kubadilisha Kilimo na Mifumo ya Chakula –** Itasaidia wanaotengeneza sera kubadilisha kilimo, ikitia ndani kupitia ruzuku na suluhisho za asili. Hazina ya AGRI3, iliyo na bilioni 1 ya dola za Marekani inayopatikana kama mkopo kwa wakulima, itategemeza urejesho wa uchumi wa baada ya COVID-19 kwa kuongeza kasi ya mabadiliko kuelekea kilimo endelevu.
- **Jumuiya ya Wafadhili wa Hali ya Hewa/ Mashirika ya Miradi ya Nguvu za Asili –** Itaandaa kichocheo kuhakikisha ahadi ya 1 Green Gigaton inafikiwa kufikia 2021, kuza Kanuni za Uwekezaji katika Suluhisho za Asili na kutegemeza mashirika kuwekeza katika suluhisho za asili. ■

*Janga hili limeonyesha udhaifu mwingi katika chumi zetu na kuongeza ubaguzi uliopo huku likionyesha umuhimu wa udhabiti, ubunifu na ushirikiano.*





ITIKIO LA KWANZA 3:

# Kuwekeza ili kujenga tena

Njia za kupunguza athari mbaya kwa mazingira inaweza kuongeza ustahimilivu kwa majanga ya wakati ujao kwa kuhakikisha mazingira yenye afya inayotegemeza watu wenye afya. Vifurushi vya kuchochea kutoka kwa hazina ya serikali ya kupunguza athari mbaya kwa mazingira na kufadhili kunaweza kutia ndani umuhimu wa kazi za kupunguza athari mbaya kwa mazingira na zenye heshima; uwekezaji kwa utajiri wa umma na jamii na miundo msingi ya ikolojia; mzunguko kuendeleza matumizi endelevu na uzalishaji; uwajibikaji kifedha kwa utulivu wa hali ya hewa na uadilifu wa ikolojia; na matokeo yanayojumuisha jamii.

Hususan, itikio la UNEP itakazia fikira:

- **Kufikia watendaji wa uchumi wa kweli ili kujenga upya, kukuza na kuongeza kasi ya matumizi endelevu na uzalishaji, na kuunda kazi mpya zinazopunguza athari mbaya kwa mazingira** –Kutegemeza upangaji bora wa uchumi na maendeleo pamoja na mifululizo jumuishi ya uzalishaji endelevu, yenye ufanisi wa rasilimali, uwajibikaji, na ustahimilivu. Hii inatia ndani kufikia biashara kupitia ushirika na mashirika ya UN, kifedha, serikali na taasisi za sekta ya kibinafsi, na kurekebisha soko na mifulululizo ya ugavi ya bidhaa zinazopunguza athari mbaya kwa mazingira na endelevu.

»

- **Kuunganisha juhudi za kurekebisha kwa kuhamia kwa nishati safi, suluhisho za msingi na Mkataba wa Paris** – Kuonyesha jinsi uwekezaji katika hali ya hewa yenye urafiki, vitendo vya asili vitachochea ukuaji wa uchumi, kutengeneza fursa za ajira, na kuongeza ustahimilivu kwa tishio za kawaida kutoka kwa wanyama. Hii inahitaji kuunganika na viumbe anuwai na agenda za hali ya hewa mapema katika mizunguko ya kupanga.
- **Kutegemeza serikali kujenga upya kizazi kijacho cha miundo msingi ya kijamii, ikolojia na uzalishaji** – Kukuza mbinu zinazotegemea mahitaji, zilizojumuishwa katika mzunguko wa maisha ya miundo msingi. Hii ni pamoja na kutegemeza mijengo ya miundo msingi endelevu, kuwazia tena miji endelevu ambayo inafaa kwa madhumuni ya ulimwengu baada ya COVID-19, na kutegemeza vifurushi endelevu vya urejeshaji wa fedha kupitia mageuzi ya fedha, dhamana ya kukuza njia za kupunguza athari mbaya kwa mazingira, na miradi mingine ya kukopesha ya umma na ya kibinafsi.

## ITIKIO LA TATU 3: SHUGHULI MUHIMU

- **Kutegemeza matendo ya nchi kuhusu ahadi ya hali ya hewa** – kutumia nishati kwa njia tofauti, uwekezaji baridi na urejeshaji ili kuioanisha na Mkataba wa Paris, katika ushirikiano na UNDP na washiriki wengine**.**
- **Kulenga sekta za kaboni ya juu na rasilimali shadidi** na vitendo ambavyo vina utajiri mkubwa wa kazi na huunganisha katika hali ya hewa, mazingira asili, na agenda za ufanisi wa rasilimali.
- **kufanya kazi na wawekezaji na Wizara ya Fedha kuhamisha uwekezaji na ruzuku** kuelekea mikakati ya asili na isiyo ya hali ya hewa, pamoja na majukwaa ya ulimwengu kama vile Net Zero Asset Alliance na Green Fiscal Policy Network



ITIKIO LA KWANZA 2:

# Kufanya usimamizi wa mazingira ya ulimwengu kuwa ya kisasa

Kupata suluhisho kwa masuala ya mazingira ni muhimu sasa kuliko wakati mwingine wowote, lakini janga limesababisha kuahirishwa kwa mikutano muhimu. Hii inasababisha kutathminiwa kwa jinsi usimamizi wa mazingira ya ulimwengu inaweza kusonga na wakati. Sekretarieti ya Mkutano juu ya Tofauti za Kibiyolojia tayari imesongesha mikutano ya kiufundi kwa jukwaa za kielektroniki. UNEP inakagua athari za kuhamisha usimamizi wa mazingira na wahusika wengi kuelekea mikutano ya kielektroniki, na hivyo kupunguza athari kwa mazingira, jukwaa za mikutano. Hususan, UNEP:

- Itafanya utafiti kuangalia mazoea ya mashirika ya serikali mbalimbali kuhusiana na mikutano ya kielektroniki- kutumia sheria za utaratibu za mikutano ya mitandao, kutoa mwelekezo na kutambulisha vizuizi na marekebisho yanayowezekana.
- Itatathmini, na kufanya kazi kushinda changamoto za vifaa za kuhamia kwenye jukwaa za mtandao.
- Panga mazoezi na wafanyakazi wanahitaji kuhakikisha kwamba UNEP na sekretarieti za Mikataba ya Mazingira ya Wahusika Wengi (MEAs) wana vifaa wanavyohitaji kutegemeza mikutano ya kielektroniki.
- Itahakikisha uratibu wa karibu na ofisi za MEAs na za Eneo UNEP inaposonga mbele na kufanya usimamizi wa mazingira ya ulimwengu kuwa ya kisasa. ■

For more information:

**unep.org**
**unep.org/covid-19-updates**

